# Maisha ya Ubikira na Matakatifu

*(Makusanyo Yaliyoandaliwa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu; Septemba 1988)*

# Maisha ya Ubikira na Matakatifu

*(Makusanyo Yaliyoandaliwa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu; Septemba 1988)*

***Kimehakikiwa na:***

*Kamati ya Uhakiki wa Tafsiri ya Kiswahili ya Kitaifa ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabahá'i wa Tanzania*

***Kimechapishwa na***

*Kamati ya Vitabu, Uchapishaji na Usambazaji ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabahá'i wa Tanzania*

*S.L.P. 585, Dar es Salaam, Tanzania.*
***Simu:*** *+255-685 637 422*

***Barua Pepe:*** *secretariat@bahai.or.tz*
*literature@bahai.or.tz*

***Toleo la: 2024***

**ISBN 978-9912-9985-2-0**

*© Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania*

Maisha hayo ya ubikira na matakatifu, pamoja na maana zake za staha, usafi, kujizuia, adabu, na nia safi, huhusisha si kingine zaidi ya kujizoeza kiasi katika yale yote yahusianayo na mavazi, lugha, burudani, na shughuli zote za kisanii na kifasihi. Yanataka hadhari ya kila siku katika kudhibiti matamanio binafsi ya kimwili na mielekeo potofu. Hutaka kuachana kabisa na mwenendo wa kipuuzi, pamoja na mwambatano wake uliokithiri kwenye starehe ndogo ndogo na aghalabu potofu. Yanahitaji kujiepusha kabisa na vinywaji vyote vya kulevya, kutokana na afyuni, na kutokana na dawa kama hizo zinazojenga mazoea. Hulaani unajisi wa sanaa na wa maandiko, matendo ya utupu na ya maisha ya uwenza, utovu wa uaminifu katika mahusiano ya ndoa, na namna zote za uasherati, za kujirahisisha, na zile za unajisi wa kingono....

*("Majilio ya Haki Takatifu" toleo la Kiingereza, (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1984), uk. 30)*

# Maisha ya Ubikira na Matakatifu

# Yaliyomo

Ukurasa

Kiwango cha Kibahá'i ……………………………………........…8

Maisha ya Ubikira na Matakatifu……….......……..................13

Nguvu ya Mfano……………………………………..............…30

## Kiwango cha Kibahá'í

### Asili ya Sheria ya Kibahá'í

Wale ambao Mungu amewajalia umaizi watatambua upesi kwamba maagizo yaliyowekwa na Mungu hufanya njia bora kabisa kwa ajili ya kudumisha utaratibu ulimwenguni na usalama wa watu wake....

Ee enyi watu wa ulimwengu! Mjue kwa hakika kwamba amri Zangu ni taa za majaliwa Yangu ya upendo miongoni mwa watumishi Wangu, na funguo za rehema Yangu kwa viumbe Vyangu. Hivyo ndivyo ambavyo zimeshushwa kutoka mbingu ya Mapenzi ya Bwana wenu, Bwana wa Ufunuo.….

Sema: Kutoka kwenye sheria Zangu harufu nzuri ya vazi Langu iweze kunuswa, na kwa msaada wake, bendera za Ushindi zitasimikwa kwenye vilele vya juu kabisa. Ulimi wa uwezo Wangu, kutoka mbingu ya utukufu Wangu wenye nguvu zote, umeuambia muumbo Wangu maneno haya: "Tiini amri Zangu kwa ajili ya upendo wa uzuri Wangu." Ni mwenye furaha yule mpenzi ambaye amevuta manukato matakatifu ya Mpendwa wake Kabisa kutoka maneno haya, yaliyosheheni marashi ya neema ambayo hakuna ulimi uwezao kuielezea. Kwa uhai Wangu! Yule ambaye amekunywa divai bora ya haki kutoka mikono ya fadhili Yangu yenye baraka tele atazungukia amri Zangu zinazong'aa juu ya Chimbuko la muumbo Wangu.

Msidhani kwamba Tumewafunulieni tu orodha ya sheria. La, bali, Tumefungua Divai bora kwa vidole vyenye uwezo na nguvu. Kwa hili hushuhudia kile ambacho Kalamu ya Ufunuo imekifunua. Taamulini juu ya hili, Enyi watu wenye umaizi!

*("Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh", toleo la marudio la Kiingereza. (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1984), kifungu. CLV, uk. 331;kurasa. 332–33)* **[1]**

Kama ambavyo kuna sheria zinazotawala maisha yetu ya kimwili, zikihitaji kwamba lazima tuilishe miili yetu vyakula fulani fulani, tuidumishe ndani ya wigo fulani wa joto, na kadhalika, kama tunataka kuepuka ulemavu wa kimwili, vivyo hivyo pia kuna sheria zinazotawala maisha yetu ya kiroho. Sheria hizi hufunuliwa kwa wanadamu katika kila zama na Mdhihirishaji wa Mungu, na utiifu kwazo ni jambo lenye umuhimu wa hali ya juu ili kila mwanadamu, na wanadamu kwa jumla, waweze kuendelea ipasavyo na kwa upatano. Zaidi ya hayo, pande hizi mbalimbali zinategemeana. Endapo mtu huvunja sheria za kiroho kwa ajili ya maendeleo yake mwenyewe si tu atasababisha madhara kwake mwenyewe bali kwa jamii ambamo yeye huishi. Vivyo hivyo, hali ya jamii ina athari ya moja kwa moja kwa watu binafsi ambao lazima waishi humo.

*(Kutoka barua ya 6 Februari 1973 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa, iliyochapishwa katika "Jumbe kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu 1968–1973" (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1976), uk. 105–6)* **[2]**

Tumezipitia barua zako kadhaa na tumetanabahi maswali yako, na mtazamo wako kwamba vijana wengi wa Kibahai huko.... wamechanganyikiwa, na wanasihi kupata mwongozo ulio katika lugha rahisi na ya wazi kuhusu jinsi ya kukabiliana na hali za kila siku, hususan zile zinazohusisha na ngono.

Haiwezekani wala haipendelewi kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kuweka vifungu vya kanuni vinavyogusia kila hali. Wala si jukumu la muumini binafsi kuamua, kulingana na uelewa wake wa kimaombi wa Maandiko, kwa hakika ni upi mwelekeo wa mwenendo wake unapaswa kuwa kuhusiana na hali ambazo anakumbana nazo katika maisha yake ya kila siku. Ikiwa inabidi atimize dhima yake kweli maishani kama mfuasi wa Ukamilifu Uliobarikiwa, atayapangilia maisha yake kulingana na Mafundisho. Muumini hawezi kulifikia lengo hili kwa kuishi tu kulingana na seti ya

kanuni zisizonyumbulika. Pale ambapo maisha yake yameelekezwa kwenye huduma kwa Bahá'u'lláh, na pale ambapo kila kitendo fahamivu hutendwa ndani ya muundo huu wa rejelea, hatashindwa kufikia kusudi la kweli la maisha yake.

Kwa hiyo, kila muumini lazima aendelee kujifunze Maandiko matakatifu na maelekezo ya mpendwa Mlinzi, akijitahidi wakati wote kufikia uelewa mpya na bora juu ya umuhimu wake kwake na kwa jamii yake. Anapaswa asali kwa bidii kwa ajili ya Mwongozo Mtakatifu, hekima na nguvu za kufanya kile kinachompendeza Mungu, na kumtumikia Yeye katika nyakati zote na kwa uwezo wake wote.

*(Kutoka barua ya 17 Oktoba 1968 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)* **[3]**

Kuhusu ubikira, hii ni mojawapo ya dhana zenye changamoto kubwa kabisa ya kuipitia katika zama hizi huria, lakini Wabahá'í lazima wafanye jitihada ya juu kabisa kushikilia viwango vya Kibaha'í, haidhuru vitaonekana vigumu kiasi gani hapo mwanzoni. Jitihada hizo zitafanywa kuwa rahisi zaidi ikiwa vijana wataelewa kwamba sheria na viwango vya Imani vimekusudiwa kuwaweka huru kutokana na magumu yasiyoelezeka ya kiroho na kimaadili kwa namna ile ile ambayo ukubalifu wa sheria za maumbile humsaidia mtu kuishi kwa upatano na nguvu za sayari.

*(Kutoka barua ya 14 Januari 1985 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)* **[4]**

**Uhuru wa Kweli**

Fikiria ufinyu wa fikra za watu. Wanaomba kile ambacho huwadhuru, na kutupilia mbali kitu ambacho huwanufaisha....

Mjue kwamba kiini cha uhuru na alama yake ni mnyama. Kile kinachomstahili mtu ni kujisalimisha kwa vile vizuizi vitakavyomkinga dhidi ya ujinga wake mwenyewe na kumlinda dhidi ya madhara ya yule mtukutu. Uhuru humfanya mtu kuvuka mipaka ya staha, na kukiuka utu wa daraja lake. Humtweza hadi kwenye kiwango cha ukengeukaji na uovu uliokithiri.

Mchukulie mtu kama kundi la kondoo linalohitaji mchungaji kwa ajili ya ulinzi wao. Huu, kwa kweli, ndiyo ukweli, ukweli yakini. Tunaidhinisha uhuru katika hali fulani fulani, na tunakataa kuuridhia katika hali zinginezo. Sisi, kwa kweli, ndiyo Wajua—Yote.

Sema: Uhuru wa kweli umo katika utiifu wa mtu kwenye amri Zangu, kidogo mlijuavyo hilo. Laiti watu wangetii kile ambacho Sisi tumewatelemshia kutoka Mbingu ya Ufunuo, hakika, wangeufikia uhuru kamili. Ni mwenye furaha yule ambaye ameelewa Kusudi la Mungu katika chochote kile Alichokifunua kutoka Mbingu ya Mapenzi Yake ambacho hupenyeza vitu vyote vilivyoumbwa. Sema: Uhuru ambao huwanufaisha ninyi haupatikani popote isipokuwa katika utumishi kamili kwa Mungu, Ukweli wa Milele. Yeyote aliyeonja utamu wake atakataa kubadilishana na milki zote za duniani na mbinguni.

*("Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh", toleo la Kiingereza, kifungu. CLIX, uk. 335–36)* **[5]**

...kuhusiana na watu wote ambao hulilia uhuru: uhuru wa kiasi ambao huuhakikishia usitawi wa ulimwengu wa binadamu na kudumisha na kuhifadhi mahusiano ya ulimwengu, hupatikana katika nguvu na mapana yake yote kwenye mafundisho ya Bahá'u'lláh.

*(“Mateuzi kutoka Maandiko ya ‘Abdu’l-Bahá” [toleo la marudio], (Haifa: Makao Makuu ya Kibahá’i ya Ulimwenguni, 1982), uk. 305)* **[6]**

## Kiwango cha Kibahá’í cha Ubikira

Wale wateule wa Mungu...hawapaswi kutazama hali ya ukengeukaji wa jamii wanamoishi, wala kwenye shuhuda za mmomonyoko wa maadili na mwenendo wa kipuuzi ambao watu wawazungukao huuonesha. Hawapaswi kujiridhisha na utofauti linganifu na ubora pekee. Bali wanapaswa wakazie macho yao kwenye vilele bora zaidi kwa kuweka mashauri na maonyo ya Kalamu ya Utukufu kama lengo lao kuu. Hapo ndipo itakapotambulika mara moja ni nyingi kiasi gani hatua ambazo zingali bado kuvukwa na ni mbali kiasi gani kutoka hapo hadi lengo litamaniwalo lilipo—lengo ambalo si lingine bali ni kielelezo cha maadili na njema za kimbingu.

*(Kutoka barua ya 30 Oktoba 1924 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Baraza la Kiroho la Mahali la Ṭihrán, iliyotafsiriwa kutoka Kiajemi)* **[7]**

Hata hivyo, lazima ikumbukwe, kwamba udumishaji wa kiwango cha juu kama hicho cha mwenendo wa kimaadili haupaswi kuhusishwa au kuchanganywa na mtindo wowote wa utawa, au wa utakatifu uliokithiri na wa kihafidhina. Kiwango kilichowekwa na Bahá’u’lláh hakitafuti, kwa hali yoyote ile, kumnyima yeyote haki na stahili yake halali kupata manufaa na faida yote kutoka kwenye furaha, uzuri, na starehe ambazo dunia imetajirishwa nazo kwa wingi mno na Muumba Mpenda-Vyote. “Iwapo mtu,” Bahá’u’lláh Mwenyewe hutuhakikishia, “angetamani kujivika mwenyewe kwa mapambo ya dunia, kuvaa mavazi yake, au kushiriki manufaa iwezayo kuyajalia, hakuna madhara yaweza kumpata, ikiwa hataruhusu chochote kile kujiingiza kati yake na Mungu, kwa kuwa Mungu ameamuru kila kitu chema, kiwe kimeumbwa mbinguni au duniani, kwa ajili ya wale kati

ya watumishi Wake ambao kwa kweli humwamini Yeye. Kuleni, Enyi watu, vile vitu vizuri ambavyo Mungu Amewaruhusu, na msijinyime wenyewe Baraka Zake za ajabu. Toeni shukrani na sifa Kwake, na muwe kati ya wale ambao kwa kweli ni wenye shukrani."

*("Majilio ya Haki Takatifu" toleo la Kiingereza, (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'i, 1984), uk. 33)* **[8]**

Kiwango cha Kibahá'í kipo juu sana, husan zaidi pale kinapolinganishwa na maadili yaliyooza kabisa ya ulimwengu wa sasa. Lakini kiwango hiki chetu kitazalisha watu wenye siha njema zaidi, furaha zaidi, bora zaidi na kuchochea ndoa imara zaidi....

*(Kutoka barua ya 19 Oktoba 1947 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)* **[9]**

## Maisha ya Ubikira na Matakatifu

### Maana yake

Maisha hayo ya ubikira na matakatifu, pamoja na maana zake za staha, usafi, kujizuia, adabu, na  nia safi, huhusisha si kingine zaidi ya kujizoeza kiasi katika yale yote yahusianayo na mavazi, lugha, burudani, na shughuli zote za kisanii na kifasihi. Yanataka hadhari ya kila siku katika kudhibiti matamanio binafsi ya kimwili na mielekeo potofu. Hutaka kuachana kabisa na mwenendo wa kipuuzi, pamoja na mwambatano wake uliokithiri kwenye starehe ndogo ndogo na aghalabu potofu. Yanahitaji kujiepusha kabisa na vinywaji vyote vya kulevya, kutokana na afyuni, na kutokana na dawa kama hizo zinazojenga mazoea. Hulaani unajisi wa sanaa na wa maandiko, matendo ya utupu na ya maisha ya uwenza, utovu wa uaminifu katika mahusiano ya ndoa, na  namna zote za uasherati, za kujirahisisha, na zile za unajisi wa kingono. Hayawezi kuvumilia wala kukubaliana na zile nadharia, viwango, tabia, na zama za uozo

wa kupindukia. La, badala yake yanatafuta kuonesha, kupitia nguvu ya kiutendaji ya mfano wake, athari za nadharia hizo, udanganyifu wa viwango hivyo, utupu wa madai hayo, upotofu wa tabia hizo, na asili ya kufuru iliyopindukia.

*("Majilio ya Haki Takatifu" toleo la Kiingereza, (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'i, 1984), uk. 30)* **[10]**

**Ubikira**

Yeye ni mfuasi Wangu wa kweli ambaye, kama akija kwenye bonde la dhahabu safi, atalipita mbali moja kwa moja kama vile wingu, na kamwe hatageuka nyuma, wala kusimama. Mtu kama huyo, kwa hakika, ni Wangu. Kutoka kwenye joho lake Umati wa Juu unaweza kuvuta manukato ya utakatifu....Na kama angekutana na mwanamke mzuri na bora kabisa kati ya wanawake, asingehisi moyo wake kushawishiwa na chembe ndogo kabisa ya kivuli cha tamaa kwa uzuri wake. Mtu kama huyo, kwa hakika, ni kiumbe wa ubikira usio na doa. Hivyo ndivyo iwaelekezavyo Kalamu ya Mkale wa Siku kama ilivyoagizwa na Bwana wenu, Mwenye Nguvu--Zote, Mwenye Baraka—Zote.

*(“Makusanyo kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh”, toleo la marudio. (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1984), sehemu. LX, uk. 118)* **[11]**

Usafi na ubikira umekuwa, na bado ungali, ndiyo mapambo makuu kabisa kwa wajakazi wa Mungu. Mungu ni shahidi Wangu! Ukali wa nuru ya ubikira humwaga mng’ao wake juu ya malimwengu ya roho, na manukato yake hupeperushwa hadi kwenye Paradiso Iliyotukuka Kabisa.

*(Bahá’u’lláh, imenukuliwa katika “Majilio ya Haki Takatifu”, uk. 32)* **[12]**

Kuhusiana na vipengele chanya vya ubikira, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu hutamka kwamba Imani ya Kibahá’í hutambua thamani ya ashiki za kingono na hushikilia kwamba asasi ya ndoa imeanzishwa kama njia ya ufanyikaji wake kiusahihi. Wabahá’í hawaamini kwamba ashiki ya kingono inapaswa kuzimwa, ila kwamba inapaswa kuwekewa utaratibu na kudhibitiwa.

Ubikira kwa vyovyote vile haumaanishi kujiondoa kwenye mahusiano ya kibinadamu. Huwaachilia huru watu kutokana na udhalimu wa mtapakao wa ngono. Mtu ambaye ana udhibiti wa ashiki zake za kingono anawezeshwa kuwa na urafiki imara na wa kudumu na watu wengi, wote wanaume na wanawake, bila hata kuuchafua lile fundo la kipekee na lenye thamani isiyokadirika ambalo linapaswa limuunganishe mume na mke.

*(Kutoka barua ya 8 Mei 1979 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)* **[13]**

**Kiasi**

Chochote kivukacho mipaka ya kiasi kitakoma kutoa ushawishi wenye manufaa. Fikiria kwa mfano vitu kama vile uhuru, ustaarabu na vingine kama hivyo. Haidhuru ni kwa kiwango gani watu wenye ufahamu watavipa kipaumbele, hatimaye, kama vikifanywa kupita kiasi, vitaleta athari yenye madhara kwa watu.

*("Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas" [toleo la marudio], (Haifa: Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwenguni, 1982), uk. 169)* **[14]**

Chaguo la mavazi na unyoaji wa ndevu na mtindo wake umeachwa katika maamuzi ya watu binafsi. Lakini jihadharini, Enyi watu, msije mkajifanya wenyewe kuwa vitu vya kuchezewa na wajinga."

*("Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas", uk. 23)* **[15]**

Matamshi ya binadamu ndiyo asili ambayo hulenga kuleta ushawishi wake na huhitaji kiasi. Kuhusu ushawishi wake, huu upo juu ya sharti la uboreshaji ambao nao hutegemea mioyo iliyojitenga na misafi. Kuhusu kiasi chake, hiki kinapaswa kichanganywa na busara na hekima kama ilivyoamriwa kwenye Maandiko na Nyaraka Takatifu.

*(“Nyaraka za Bahá’u’lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas”, uk. 172)* **[16]**

Tumewaruhusu kusikiliza muziki na kuimba. Jihadharini walakini, usikilizaji huo usije ukawafanya muvuke mipaka ya staha na heshima. Shangilieni kwa shangwe ya Jina Langu Kuu Kabisa ambalo kupitia hilo mioyo inachangamshwa na akili za wale waliopendelewa kuvutiwa....

*(Kutoka Kitáb-i-Aqdas)* **[17]**

Katika mafundisho hakuna chochote kinachopinga kucheza muziki, lakini marafiki wanapaswa kukumbuka kwamba kiwango cha Bahá’u’lláh ni staha na ubikira. Mazingira ya kumbi za kisasa za muziki, ambako uvutaji na unywaji na uasherati uliopindukia huendelea kufanyika, ni mabaya sana, lakini uchezaji wa kistaarabu wenyewe hauna madhara. Kwa hakika hakuna madhara katika ucheza muziki wa jadi au kujifunza muziki shuleni. Pia hakuna madhara kushiriki katika maigizo. Vivyo hivyo katika uigizaji wa sinema. Kitu kinachodhuru, siku hizi, siyo sanaa yenyewe bali upotoshaji wa bahati mbaya ambao mara nyingi huzizingira sanaa hizi. Kama Wabahá’í hatuhitaji kuiepuka yoyoye miongoni mwa sanaa hizi, bali matendo na mazingira ambayo wakati mwingine huambatana na taaluma hizi ndiyo tunapaswa tuyaepuke.

*(Kutoka barua ya 30 Juni 1952 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa Baraza moja la Kiroho la Kitaifa)* **[18]**

## Hadhari ya Vitendo vya kila Siku

Inukeni, Enyi watu, na, kwa nguvu ya uwezo wa Mungu, mdhamirie kupata ushindi juu ya nafsi zenu wenyewe, ili pengine dunia yote iweze kuachiliwa huru na kutakaswa kutoka utumwa wake kwa miungu yake ya mawazo ya bure—miungu ambayo imewasababishia upotevu kama huo, na inawajibika kwa mateso ya waabudu wao

dhalili. Sanamu hizi zinaweka kizuizi ambacho humkinza mtu katika jitihada zake kusonga mbele kwenye njia ya ukamilifu.

*("Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh", toleo la Kiingereza, sehemu XLIII, uk. 93)* **[19]**

EWE MWANA WA KUWA!

Jifanyie hesabu mwenyewe kila siku kabla hujaitwa kwenye kutoa hesabu; kwa kuwa kifo, bila onyo, kitakufikia na utaitwa kutoa hesabu ya matendo yako.

*("Maneno Yaliyofichwa ya Bahá'u'lláh", toleo la marudio (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1985), Kiarabu na. 31, uk. 9* **[20]**

Kwa kuwa tamaa ni mwale ambao umeteketeza hadi kuwa majivu mavuno yasiyohesabika ya maisha yote ya wasomi, moto ushambuliao ambao hata bahari kubwa ya maarifa yao yaliyolundikana kamwe usingeweza kuuzima. Ni mara ngapi imetokea kwamba mtu ambaye alikuwa ameneemeshwa na kila sifa ya kibinadamu na kuvaa lulu ya ufahamu wa kweli, bado alipozifuata shauku zake hadi sifa zake bora kabisa zikavuka kiasi na akalazimishwa kuzidi. Nia zake safi zikabadilika kuwa ovu, sifa zake hazikuweza tena kufaa kwa matumizi yanayozistahili, na nguvu ya tamaa zake ikamgeuzia kando ya unyofu na thawabu zake zikawa njia hatarishi na zenye giza. Tabia njema machoni pa Mungu na wateule Wake na wale wenye umaizi, ndiyo iliyo bora na ya kusifika kabisa kati ya vitu vyote, lakini mara nyingi kwa sharti kwamba chimbuko la utokeaji wake linapaswa kuwa mantiki na maarifa na msingi wake unapaswa uwe ukadirifu wa kweli.

*("Siri ya Ustaarabu Mtakatifu", toleo la pili (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1983), uk. 59–60)* **[21]**

**Kuachana na Mwenendo wa Kipuuzi**

EWE RAFIKI YANGU!

Wewe u nyota mchana ya mbingu za utakatifu Wangu, usiache najisi ya dunia iufunike wangavu wako. Raruria mbali utando wa uzembe, ili kutoka nyuma ya mawingu uweze kuibuka mwangavu na uvivike vitu vyote kwa vazi la uzima.

*("Maneno Yaliyofichwa ya Bahá'u'lláh", Kiajemi na. 73, uk. 46)* **[22]**

Jiwekeni huru kutokana na mwambatano kwa ulimwengu huu na ubatili wake. Jihadharini msije mkavisogelea, kwa kuwa vinawashawishi kuenenda kufuatana na tamaa zenu wenyewe na matamanio yenye uchu wenye, na kuwazuia kuingia katika Njia iliyonyooka na tukufu.

*("Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh", toleo la Kiingereza, sehemu. CXXVIII, uk. 276)* **[23]**

Kwenye ukurasa wa 25[1] wa "Majilio ya Haki Takatifu" mpendwa Mlinzi akielezea mahitaji siyo tu ya ubikira, bali ya "maisha ya ubikira na matakatifu"—vivumishi vyote viwili ni muhimu. Mojawapo ya ishara za jamii iliyooza, ishara ambayo iko wazi sana katika ulimwengu leo, ni ile ibada yenye wazimu inayokaribiana na starehe na ukengeukaji, kiu isiyotosheka ya burudani, ibada ya kishabiki kwa michezo na burudani, kukaidi kulitilia uzito jambo lolote, na mwelekeo wa dharau, dhihaka kwa njema na vile vinavyostahili thamani. Uachaji wa "mwenendo wa kipuuzi" haumaanishi kwamba Mbahá'í lazima awe na kisirani au mnyoofu daima. Ucheshi, furaha, shangwe ni sifa za maisha halisi ya Kibahá'í. Mambo yasiyo na maana na yanayokinaisha mwishowe husababisha ukinaifu na utupu, lakini furaha ya kweli na shangwe na ucheshi ambavyo ni

---

[1]*Kwenye ukureasa wa 25 katika toleo la 1956 la U.S.; ukurasa 30 katika toleo la 1984 la U.S.*

sehemu za maisha yenye uwiano ambayo hujumuisha mawazo yenye maana, huruma na utumishi mnyenyekevu kwa Mungu, ni sifa zinazositawisha maisha na kuongezea kwenye uchangamfu wake.

Uchaguzi wa maneno wa Shoghi Effendi mara nyingi ulikuwa wa maana, na kila moja ni la muhimu katika kuelewa mwongozo wake. Katika aya hii mahsusi, hakatazi starehe “ndogo ndogol”, bali huonya dhidi ya “mwambatano uliokithiri” kwazo na huonesha kwamba mara nyingi zinaweza “zikapotoshwa”. Mtu anakumbushwa kuhusu tahadhari ya ‘Abdu’l-Bahá’ kwamba tusiruhusu burudani kugeuka kuwa upotezaji wa muda.

*(Kutoka barua ya 8 Mei 1979 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)* **[24]**

**Pombe**

Muwe wenye kuleweshwa kwa divai ya upendo wa Mungu, na siyo kwa ile ambayo hufisha fikra zenu, Ee nyinyi mnaomhusudu Yeye! Kwa kweli, imekatazwa kwa kila muumini, awe mwanaume au mwanamke.

*(Bahá’u’lláh, imenukuliwa katika “Majilio ya Haki Takatifu”, uk. 33)* **[25]**

Unywaji wa divai, kulingana na maandiko ya Kitabu Kitakatifu Kabisa, umekatazwa; kwa kuwa ni chanzo cha maradhi ya kukubuhu, hudhoofisha mishipa ya fahamu, na huteketeza akili.

*(‘Abdu’l-Bahá, imenukuliwa katika “Majilio ya Haki Takatifu”,uk. 33)* **[26]**

**Dawa za Kulevya**

Kuhusu afyuni, ni ya kuchukiza na imelaaniwa. Mungu atulinde kutokana na adhabu aitoayo kwa mtumiaji. Kwa mujibu wa Maandiko dhahiri ya Kitabu Kitakatifu Kabisa, imekatazwa, na matumizi yake yamelaaniwa kabisa. Mantiki huonesha kwamba uvutaji wa afyuni ni aina ya wendawazimu, na tajiriba huthibitisha kwamba mtumiaji anakuwa ametengwa kabisa kutoka milki ya kibinadamu. Mungu na awalinde wote dhidi ya kutenda kitendo kibaya mno kama hiki, kitendo ambacho huuangamiza kabisa msingi hasa wa kile ambacho kinapaswa kuwa ndiyo ubinadamu, na ambacho husababisha mtumiaji kunyimwa milele na milele. Kwa sababu afyuni hujing'ang'aniza kwenye roho kiasi kwamba dhamiri ya mtumiaji hufa, akili yake huondoshwa, utambuzi wake humomonyolewa. Inamgeuza aliye hai kuwa mfu. Inazima joto la kiasili. Hakuna madhara makubwa zaidi yanayoweza kufikiriwa kuliko yale yanayoletwa na afyuni. Wana bahati wale ambao kamwe hawataji hata jina lake, basi fikiria jinsi gani alivyo dhalili mtumiaji.

*("Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá" [toleo la marudio], (Haifa: Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu, 1982), uk. 148–49)* **[27]**

Kuhusu hashish umetaja kwamba baadhi ya watu wa Uajemi wamekuwa na uraibu na utumiaji wake. Mungu wa Rehema! Hiki ni kibaya kabisa kuliko vilevi vyote, na katazo lake limefunuliwa wazi wazi. Matumizi yake husababisha mmomonyoko wa fikra na unyogovu kabisa wa roho. Inawezekanaje mtu atafute tunda la mti wa jahanam, na kwa kulila, ajipambanue kwa sifa za jinamizi? Inawezekanaje mtu atumie dawa hii iliyokatazwa, na hivyo kujinyima mwenyewe baraka za Mwenye Rehema Zote?

Kilevi huteketeza akili na kumfanya mtu kutenda vitendo vya kipuuzi, lakini afyuni hii, tunda hili la kuchukiza la mti wa jahanam, na hashish hii ovu huzimisha akili, hugandisha roho, huigeuza roho kuwa jiwe, huharibu mwili na kumuacha mtu aliyefadhaishwa na kupotea.

*(‘Abdu’l-Bahá, kutoka Waraka—uliotafsiriwa kutoka Kiajemi)*
**[28]**

Kuhusu zile ziitwazo njema za “kiroho” dawa za halusinogeni (dawa za usingizi),...uamsho wa kiroho unapaswa utokee kwa mtu kugeuzia moyo wake kwa Bahá’u’lláh, na siyo kupitia njia za kimwili kama vile dawa na viambata. Kutokana na maelezo yaliyotolewa kwenye barua yako inaonekana kwamba viambata vya halusinogeni ni aina ya kilevi. Kwa vile marafiki, wakiwemo vijana, wanatakiwa hasa wajiepushe na aina zote za vilevi, na zaidi wanategemewa kwa uaminifu kutii sheria za kiraia za nchi yao, ni dhahiri kwamba wanapaswa kujizuia na utumiaji wa dawa hizi.

Jukumu kubwa kabisa kwa amani na usitawi wa siku zijazo za ulimwengu limebebwa na vijana wa leo. Acha vijana wa Kibahá’í kwa nguvu ya Hoja wanayoitetea wawe mfano ung’aao kwa wenzi wao.

*(Kutoka barua ya 15 Aprili 1965 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Baraza moja la Kiroho la Kitaifa)*
**[29]**

Wabahá’í wasitumie viambata vya hallusinogeni, ikiwemo LSD (lysergic acid diethylamide), peyote na dutu za namna hiyo, isipokuwa pale zinapoelekezwa kwa ajili ya matumizi ya kitabibu. Wala wasijihusishe na majaribio ya dutu kama hizo.

*(Kutoka barua ya 11 Januari 1967 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Baraza moja la Kiroho la Kitaifa)*
**[30]**

## Mtazamo wa Kibahá'í Kuhusu Ngono

Imeelezwa kwa ufupi kwamba dhana ya Kibahá'í juu ya ngono imeegemezwa juu ya imani kwamba ubikira lazima utekelezwe ipasavyo na jinsi zote mbili, si tu kwa sababu jambo lenyewe hustahili sifa kimaadili, bali pia kwa sababu ndiyo njia pekee kwa ajili ya maisha yenye furaha na mafanikio ya ndoa. Kwa hiyo uhusiano wa kingono wa aina yoyote, nje ya ndoa, hauruhusiwi, na yeyote akiukaye kanuni hii si tu atawajibika mbele ya Mungu, bali atapewa adhabu anayostahili kutoka kwa jamii.

Imani ya Kibahá'í hutambua thamani ya ashiki za ngono, lakini hulaani udhihirisho wake usio halali na usiofaa kama vile mapenzi huria, uwenza na zinginezo, ambapo zote huchukuliwa kuwa zenye madhara kwa mtu na jamii ambamo yeye huishi. Matumizi yafaayo ya hisia za ngono ni haki ya kiasili ya kila mmoja, na ni hasa kwa kusudi hili hili kwamba shirika la ndoa limeanzishwa. Wabahá'í hawaamini katika ukandamizaji wa ashiki ya ngono bali katika urekebishaji na udhibiti wake.

*(Kutoka barua ya 5 Septemba 1938 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)* **[31]**

Kuhusu swali lako iwapo kuna namna zozote za udhihirisho wa ashiki ya ngono ambazo ni halali nje ya ndoa; kulingana na mafundisho ya Kibahá'í hakuna tendo la kingono linaweza kufikiriwa kuwa halali isipokuwa likitendwa kati ya watu waliooana kihalali. Nje ya maisha ya ndoa hapawezi kuwa na matumizi halali au yenye afya ya ashiki ya ngono. Vijana wa Kibahá'í, kwa upande mmoja, wanapaswa wafundishwe somo la kudhibiti nafsi ambalo, linapotekelezwa, bila shaka huwa na manufaa kiafya katika maendeleo ya tabia na haiba kwa jumla, na kwa upande mwingine wanapaswa washauriwe, la, hata kutiwa moyo, kufunga ndoa wangali bado vijana na wenye nguvu kamili za ujana. Vigezo vya kiuchumi, bila shaka, mara nyingi huwa kikwazo kikubwa kwa ndoa

za mapema, lakini katika hali nyingi hivi ni visingizio tu, na kwa hivyo havipaswi kuendekezwa.

*(Kutoka barua ya 13 Desemba 1940 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)* **[32]**

Ubikira humaanisha vyote viwili kabla na baada ya ndoa yawepo maisha yasiyo na mawaa, ya ubikira. Kabla ya ndoa ubikira kamili, baada ya ndoa uaminifu kamili kwa mwenzi uliyemchagua. Uaminifu katika vitendo vyote vya ngono, uaminifu katika maneno na matendo.

Leo ulimwengu umezamishwa, miongoni mwa mambo mengine, katika upigaji chuku uliopitiliza wa umuhimu wa mapenzi ya kimwili, na upungufu wa tunu za kiroho. Kwa kadiri iwezekanavyo waumini wanapaswa wajaribu kulitambua hili na kuinuka juu ya upeo wa wenzao ambao, kwa kawaida katika vipindi vyote vya uozo katika historia, wanaweka msisitizo wa hali ya juu mno kwenye upande wa kukutana kimwili tu. Nje ya maisha yao ya kawaida ya ndoa halali wanapaswa watafute kuanzisha mafundo ya uswahiba na upendo ambavyo ni vya milele na msingi wake upo kwenye maisha ya kiroho ya mtu, siyo kwenye maisha yake ya kimwili. Hii ni moja ya nyanja nyingi ambamo Wabahá'í hawana budi kuweka mfano na kuongoza njia kwenye kiwango cha kweli cha maisha ya binadamu, ambapo roho ya mtu inatukuzwa na mwili wake ni chombo tu cha roho yake iliyoongoka. Haina haja kusema, hili haliondoi kuishi maisha makamilifu ya kawaida ya ngono katika njia yake halali ya ndoa.

*(Kutoka barua ya 28 Septemba 1941 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)* **[33]**

## Vitendo Visivyo vya Kimaadili Vimelaaniwa

Mmekatazwa kufanya uzinzi, ulawiti na ukware. Viepukeni hivyo, Enyi umati wa waaminifu. Kwa haki ya Mungu! Mmeitwa kwenye uhai kuusafisha ulimwengu kutokana na unajisi wa shauku za uovu. Hiki ndicho kile Bwana wa wanadamu wote ameakigiza juu yenu, laiti mngelitambua hilo. Yule ambaye hujihusisha kwa Mwenye-Rehema Kabisa na akafanya vitendo vya kishetani, kwa kweli huyo siyo Wangu. Kwa hili kila chembe, changarawe, mti na tunda, na zaidi ya hivyo Ulimi huu utangazao daima, mkweli na uaminikao hushuhudia.

*(Bahá'u'lláh, kutoka Waraka—uliotafsiriwa kutoka Kiarabu)* **[34]**

Tunapotambua kwamba Bahá'u'lláh husema uzinzi hudhoofisha maendeleo ya roho baada ya kifo—hii inahuzunisha mno—na kwamba unywaji huharibu akili, na tusiukaribie kabisa, tunaona yalivyo bayana mafundisho yetu juu ya masuala haya.

*(Kutoka barua ya 30 Septemba 1949 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)* **[35]**

Miongoni mwa maovu mengine mengi yanayoitesa jamii katika alama hii ya chini ya kiroho katika historia ni suala la utovu wa maadili, na msisitizo uliopitiliza wa ngono. Mapenzi ya jinsia moja, kulingana na Maandiko ya Bahá'u'lláh, kiroho umelaaniwa. Hii haimaanishi kwamba watu walioathirika sana navyo lazima wasisaidiwe na kushauriwa na kuonewa huruma. Haimaanishi kwamba sisi hatuamini kwamba huo ndio mtindo ulioruhusiwa wa maisha; ambao, chonde chonde, ndiyo mwelekeo unaokubalika mara nyingi siku hizi.

Lazima tupambane dhidi ya maovu katika jamii kwa njia za kiroho, na kwa njia za kitabibu na kijamii vile vile. Lazima tuwe

wavumilivu lakini tusioyumba, waelewa lakini thabiti kwenye mtazamo wetu.

*(Kutoka barua ya 21 Mei 1954 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)* **[36]**

Matatizo kadhaa ya kingono, kama vile mapenzi ya jinsia moja na yale ya kubadili jinsia yanaweza pia kuwa sehemu ya matibabu, na katika hali kama hizo, nafuu hiyo kwa hakika inabidi ipatikane kwa msaada bora kabisa wa kitabibu. Lakini iko wazi kutoka mafundisho ya Bahá'u'lláh kwamba mapenzi ya jinsia moja siyo hali ambayo kwayo mtu anapaswa kuridhika nayo, bali ni uvurugaji wa asili yake ambao unapaswa udhibitiwe na kushindwa. Hili linaweza kuhitaji jitihada kubwa, lakini hiyo hiyo pia ndiyo jitihada inayoweza kuhitajika na mtu anayevutiwa na jinsia tofauti ili kuzidhibiti ashiki zake. Zoezi la kujidhibiti nafsi katika hili, kama ilivyo katika nyanja nyingi mno za maisha, lina athari zenye manufaa kwenye maendeleo ya roho. Inafaa, zaidi ya hayo, ifahamike kwamba ingawa kuoana kunapendelewa sana, na Bahá'u'lláh amelitilia sana mkazo, hilo siyo kusudi kuu la maisha. Ikiwa mtu atasubiri kipindi fulani kabla ya kumpata mwenzi, au ikiwa hatimaye, ni lazima abakie pekee, haimaanishi kwamba kwa kufanya hivyo hawezi kutimiza kusudi lake la maisha.

*(Kutoka barua ya 6 Februari 1973 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa, ilichapishwa katika "Jumbe kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu 1968–1973" (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1976), uk. 110–11)* **[37]**

Barua yako iliyokuwa ikiomba marejeleo ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja katika Maandiko ya Imani kuhusu ubakaji au ukatili wa kingono ilipelekwa kwa Idara ya Utafiti, na tumeombwa kuwasilisha kwako maoni yafuatayo.

“Ukware” ni dhahiri umekatazwa na Bahá’u’lláh (tazama “Waraka kwa Mwana wa Mbwamwitu”, toleo la Kiingereza, uk. 49), na Shoghi Effendi ameeleza kwamba “maisha ya ubikira na matakatifu”, kulingana na Mafundisho ya Imani, humaanisha ukemeaji wa “tabia zote” za “unajisi wa kingono*”.*

*(Tazama “Majilio ya Haki Takatifu”,toleo la Kiingereza, uk. 25.)*[2]

Na kwa mujibu wa maudhui ya Kitáb-i-Aqdas, moja ya maagizo ya Kitabu hicho Kitakatifu Kabisa ni “mtu kutoziendekeza tamaa zake” (tazama “Ufupisho na Mpangilio wa Sheria na Maagizo ya Kitáb-i-Aqdas”, uk. 50). Aidha, marejeleo yanapaswa yafanywe kwenye moja ya “makatazo” yaliyotajwa kwenye ukurasa wa 47 wa “Ufupisho”,yaani “uzinzi”. Neno hili hutokea hivyo katika kitabu hiki kwa sababu vipengele vilivyoingizwa kwenye ufupisho lazima vihitaji kufupishwa, na kwa neno chanzi lililotumiwa na Bahá’u’lláh katika Aqdas, yaani., “ziná”, uzinzi kwa jumla na kwa kiasi kikubwa ndilo lililokusudiwa. Hata hivyo, hili kwa vyovyote vile haligusii maana *zote za dhana ya* “ziná” katika lugha ya kisheria itumikayo katika Kiarabu na Kiajemi. Mojawapo ya aina za “ziná”—yaani, pale ambapo tendo la kingono lisilo halali linatendwa kwa nguvu au ukatili—ni ubakaji au ukatili wa kingono.

Na kuhusu adhabu kwa vitendo kama vile ubakaji, hizi zitakuja kuamriwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

*(Kutoka barua ya 8 Juni 1982 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)* **[38]**

---

[2]*On page 25 in the 1956 U.S. Edition; on page 30 in the 1984 U.S. edition.*

**Matumizi ya Kanuni za Maisha ya Ubikira na Matakatifu**

...[ubikira kamili] kwa kiasi kikubwa na moja kwa moja unahusiana na vijana wa Kibahá'í, ambao wanaweza kuchangia kwa uwazi kabisa kwenye uhodari, usafi, na nguvu iongozayo maisha ya jumuiya ya Kibahá'í, na ambao juu yao lazima utegemee mwelekeo wa siku zijazo wa hatima yake, na ukunjukaji kamili wa vipawa ambavyo kwayo Mungu Ameijalia....

Na kuhusu maisha ya ubikira na matakatifu, hayapaswi kuchukuliwa kama kigezo kisicho muhimu ambacho lazima kichangie fungu lake stahiki kwenye uimarishaji na uhuishaji wa jumuiya ya Kibahá'í, ambayo kwayo kwa upande wake lazima ufanisi wa mpango au shughuli yoyote za Kibahá'í utegemee.... Wote kwa pamoja, wawe wanaume au wanawake, lazima, katika saa hii ya kutisha ambapo miangaza ya dini inafifia, na vikwazo vyake vinatokomezwa kimoja baada ya kingine, watulie na wajitathmini wenyewe, waichunguze mienendo yao, na kwa azimio lenye dhamira safi wainuke kuyatakasa maisha ya jumuiya yao dhidi ya kila dalili ya unyogovu wa kimaadili iwezayo kulitia doa jina, au kuuharibu uadilifu, wa hii Imani takatifu na ya thamani mno.

Maisha ya ubikira na matakatifu lazima yafanywe kuwa kanuni iongozayo katika tabia na mwenendo wa Wabahá'í wote, kwa pande zote mbili katika mahusiano yao ya kijamii na wana-jumuiya yao wenyewe, na katika kukutana kwao na ulimwengu kwa jumla. Lazima yazipambe na kuziimarisha jitihada zisizokoma na juhudi stahilifu za wale ambao daraja lao la kuenziwa ni kuutangaza Ujumbe, na kuyasimamia shughuli za Imani ya Bahá'u'lláh. Lazima yadumishwe, katika uadilifu na maana zake zote, katika kila hatua ya maisha ya wale ambao wanaojaza safu za Imani hiyo, wawe nyumbani mwao, safarini mwao, katika vilabu vyao, katika vyama vyao, katika burudani zao, shuleni kwao, na vyuoni mwao. Lazima yapewe uzito maalum katika uendeshaji wa shughuli za kijamii za kila shule ya kiangazi ya Kibahá'í na matukio mengine

yoyote ambapo maisha ya jumuiya ya Kibahá'í yamepangiliwa na kukuzwa. Lazima kwa ukaribu na kwa uendelevu yatambulishwe na dhima ya vijana wa Kibahá'í, kwa yote mawili; kama msingi katika maisha ya jumuiya ya Kibahá'í, na kama kigezo katika maendeleo na mwelekeo wa siku zijazo wa vijana kuhusu nchi yao wenyewe.

*("Majilio ya Haki Takatifu", toleo la Kiingereza, uk. 22; uk. 29–30)* **[39]**

## Nguvu ya Mfano

### Tabia Istahiliyo Sifa

Yeyote ainukaye, katika Siku hii, kuisadia Hoja Yetu, na akayaita kwa ajili ya kumsaidia majeshi ya tabia istahiliyo sifa na mwenendo mnyofu, ushawishi utiririkao kutokana na kitendo kama hicho, kwa uhakika kabisa, utatawanywa kote ulimwenguni.

*("Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh", toleo la marudio la Kiingereza, (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'íi, 1984), sehemu. CXXXI, uk. 287)* **[40]**

Mbahá'í anajulikana kwa sifa zidhihirishwazo naye, siyo kwa jina lake: yeye anatambuliwa kwa tabia yake, siyo kwa mwonekano wake.

*('Abdu'l-Bahá, kutoka Waraka—uliotafsiriwa kutoka Kiajemi)* **[41]**

...kwa kutii sheria ya Kibahá'í katika kukabiliana na shida zote si tu tunaimarisha tabia zetu wenyewe bali tunawashawishi wale watuzungukao.

*(Kutoka barua ya 6 Februari 1973 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa, iliyochapishwa kwenye "Jumbe kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu 1968–1973" (Wilmette: Shirika la Uchapishaja la Kibahá'í 1976), uk. 107)* **[42]**

### Umuhimu wa Matendo

EWE MWANA WA KIJAKAZI WANGU!

Uongozi daima umekuwa ukitolewa kwa maneno, na sasa unatolewa kwa matendo. Kila mmoja lazima aoneshe dhahiri

matendo ambayo ni safi na matakatifu, kwa kuwa maneno ni mali ya wote sawa sawa, ambapo matendo kama haya ni mali ya wapendwa Wetu tu. Jibidisheni basi kwa moyo na roho kujipambanua wenyewe kwa matendo yenu. Kwa namna hii Sisi tunawaasa katika waraka huu mtakatifu na ung'aao.

*("Maneno Yaliyofichwa ya Bahá'u'lláh", toleo la marudio. (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'i, 1985), Kiajemi Na. 76, uk. 47)* **[43]**

Kitendo kimoja kinyofu kimejaliwa nguvu ambayo inaweza kuliinua sana vumbi kiasi cha kulifanya livuke mipaka ya mbingu ya mbinguni. Linaweza kulirarulia mbali kila fundo, na lina nguvu ya kuirejesha kani ambayo imejimaliza yenyewe na kutoweka....

Muwe wasafi, Enyi watu wa Mungu, muwe wasafi; muwe wanyofu, muwe wanyofu....

*("Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh", toleo la Kiingereza, sehemu. CXXXI,uk. 287)* **[44]**

Mlinzi amehimiza, tena na tena, umuhimu wa lazima kwa Vijana wa Kibahá'í kuonesha Mafundisho kwa vitendo, hususan kabisa ule upande wao wa kimaadili. Ikiwa hawatajipambanua kwa mwenendo wao uliotukuka, hawawezi kutarajia vijana wengine waichukulie Hoja kwa uzito mkubwa.

Kwa moyo mkunjufu yeye anakubaliana nanyi kwamba vinginevyo tunayaweka Mafundisho katika vitendo hatuwezi kutarajia Imani kukua, kwa sababu kusudi la kimsingi la dini zote—ikiwemo yetu wenyewe—ni kumsogeza mtu karibu zaidi na Mungu, na kubadilisha tabia yake, ambayo ndiyo ya umuhimu wa hali ya juu kabisa. Msisitizo uliopindukia mara nyingi huwekwa kwenye nyanja za Mafundisho ya kijamii na kiuchumi; lakini uwanja wa kimaadili hauwezi kusisitizwa zaidi.

*(Kutoka barua ya 6 Septemba 1946 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini binafsi)* **[45]**

## Matokeo ya Mfano

Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwa kupitia matendo safi na mema, kupitia mwenendo usifikao na unaostahili.

*(Bahá'u'lláh, imenukuliwa katika "Majilio ya Haki Takatifu" (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1984), uk. 24–25)* **[46]**

Acheni matendo yenu yawe mwongozo kwa wanadamu wote, kwa kuwa shughuli za watu wengi mno, wawe wa hali ya juu au ya chini zinatofautiana na mwenendo wao. Ni kupitia matendo yenu kwamba mnaweza kujipambanua wenyewe kutoka kwa wengine. Kupitia kwayo mwangaza wa nuru yenu uweze kuangaziwa juu ya dunia nzima. Ni mwenye furaha mtu yule ambaye husikia ushauri Wangu, na huzingatia maonyo yaliyotolewa na Yeye Ambaye ni Mjua—Yote, Mwenye Hekima—Kabisa.

*("Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh", toleo la Kiingereza, sehemu. CXXXIX, uk. 305)* **[47]**

Hizi ndizo siku za kuipatia Hoja takatifu ushindi na msaada wenye ufanisi! Ushindi wa Imani ya Mungu hutegemea juu ya ufundishaji; na ufundishaji sharti utegemee vitendo vinyofu na matendo na mwenendo mwema. Jiwe la msingi la maisha ya kuishi katika njia ya Mungu ni utafutaji wa ubora wa kimaadili na upataji wa tabia zilizojaliwa sifa zinazopendeza machoni Pake. Wabahá'í wanawapaswa wajipambe kwa joho hili takatifu; kwa upanga huu wenye uwezo mkuu inabidi wazishinde ngome za mioyo ya watu. Watu wamechoshwa na hawana subira kwa balagha na mijadala, kwa mahubiri na mihadhara ya kidini. Katika siku hii, kitu pekee kinachoweza kuukomboa ulimwengu kutoka kwenye maumivu yake na kuvutia mioyo ya watu wake ni matendo, siyo maneno; mfano,

siyo mawaidha; njema za kitakatifu, siyo matamko na mikataba itolewayo na serikali na mataifa kuhusu mambo ya kijamii na kisiasa. Katika mambo yote, makubwa au madogo, neno lazima lishamirishane na kitendo, na kitendo kiwe mwenzi wa neno: kila kimoja lazima kikijalize, kikisaidie na kikiimarishe kingine. Ni kwa njia hii kwamba Wabahá'í lazima watafute kujipambanua...

*(Kutoka barua ya 8 Desemba 1923 iliyoandikwa na Shoghi Effendi kwa Wabahá'í huko Bombay—imetafsiriwa kutoak Kiajemi)* **[48]**

Kimsingi ni kupitia nguvu ya matendo bora na tabia, kuliko kupitia nguvu ya maelezo na mathibitisho kwamba marafiki wa Mungu wanapaswa waudhihirishie ulimwengu kwamba kile kilichoahidiwa na Mungu hakina budi kutokea, kwamba tayari kinafanyika na kwamba habari njema takatifu za furaha zipo wazi, dhahiri na kamilifu. Kwa kuwa hadi pale roho kadhaa zenye ubora usio kifani zitakapojitokeza mbele kuingia kwenye uga wa huduma na kujitofautisha kwa mng'ao wao mbele ya umati wa watu, kazi ya kuthibitisha ukweli wa Hoja hii machoni pa watu walioongoka ingekuwa ya kuogofya kwa hakika. Hata hivyo, ikiwa marafiki watakuwa mifano halisi ya njema na tabia nzuri, maneno na mabishano yatakuwa hayana umuhimu. Matendo yao yenyewe yatatumika kama ushuhuda thabiti, na mwenendo wao bora utahakikisha hifadhi, uadilifu na utukufu wa Hoja ya Mungu.

*(Kutoka barua ya 19 Desemba 1923 kutoka kwa Shoghi Effendi kwenda kwa Wabahá'í wa Mashariki—imetafsiriwa kutoka Kiajemi)* **[49]**

Hakuna shaka kwamba kiwango cha ubikira usio na doa kilichohimizwa na Bahá'u'lláh katika mafundisho Yake kinaweza kufikiwa na marafiki pale tu wanaposimama imara na kwa ujasiri kama wafuasi wasioyumba wa mtindo wa maisha ya Kibahá'í, wakiwa na ufahamu kamili kwamba wanawakilisha mafundisho ambayo ni kinyume kabisa na zile nguvu za uharibifu ambazo bila

huruma zinaendelea kuziharibu mfumo wa tunu za maadili ya mtu. Mwenendo uliopo katika jamii ya kisasa na mgogoro kati yake na misingi yetu ya mwenendo wa kimaadili inayoleta changamoto, mbali na kuwashawishi waumini kulegeza azma yao ya kushikilia bila kukengeuka viwango vya usafi na ubikira vilivyowekwa na Imani yao kwa ajili yao, lazima viwachochee kuyabeba wajibu wao mtakatifu kwa dhamira thabiti na hivyo kuzishambulia nguvu za uovu zinazoidumaza misingi ya maadili ya mtu.

*(Kutoka barua ya 22 Mei 1966 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa muumini binafsi)* **[50]**

Ni jukumu lenye changamoto kwa Wabahá'í kuitii sheria ya Mungu katika maisha yao wenyewe, na pole pole kuwashinda wanadamu waliobakia kwenye kukubalika kwake.

Katika kuyafikiria matokeo ya utiifu wa sheria katika maisha binafsi, mtu lazima akumbuke kwamba kusudi la maisha haya ni kuiandaa roho kwa yale yajayo. Hapa mtu lazima ajifunze kuzidhibiti na kuziongoza hisia zake za kinyama, kutokuwa mtumwa kwazo. Maisha katika ulimwengu huu ni mfuatano wa majaribu na mafanikio, ya kukosa kufikia malengo na ya kupiga hatua mpya ya maendeleo ya kiroho. Nyakati zingine njia yaweza kuonekana ngumu sana, lakini mtu anaweza kushuhudia, tena na tena, kwamba ile roho iliyosimama thabiti kutii sheria ya Bahá'u'lláh, hata ionekane ngumu kiasi gani, hukua kiroho, ambapo ile inayolegeza sheria kwa ajili ya furaha yake yenyewe ipitayo huonekana kama iliyokuwa ikifuata njozi: Yeye haifikii ile furaha aliyoitafuta, huyarudisha nyuma maendeleo yake ya kiroho na mara nyingi hujiletea mwenyewe matatizo mapya.

*(Kutoka barua ya 6 Februari 1973 iliyoandikwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa, iliyochapishwa katika "Jumbe kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu 1968–1973" (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'i 1976), uk. 106)* **[51]**